**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Itikadi Katika Tamthilia za Kifo Kisimani (2001) na Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2004)

*Minyade Sheril Mugaduka[1*] na Jessee Murithi[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100 Nairobi, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0001-6902-1895; Barua pepe ya mawasiliano: minyadesheril@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*14 Aprili 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Itikadi, umwinyi, Usemi, Ubepari, Uchanganuzi Tahakiki Usemi.*

**IKISIRI**

Itikadi ni mawazo na fikra zinazohalalisha masuala katika kijamii. Fikra hizi huhalalisha mamlaka ya kisiasa na seti za matendo zinazotekeleza vitendo. Itikadi hupata mamlaka na uhalali kwa hiari bila kutumia nguvu. Viongozi wa kisiasa na kidini hujiegemeza katika itikadi fulani ili kufanikisha malengo yao kwa sababu wanafahamu kuwa itikadi hiyo imekubalika na wanajamii. Mabadiliko hayawezi kuepukika, na jinsi sekta tofauti tofauti katika jamii zinapopitia mabadiliko ndivyo viongozi wanavyobadilisha mbinu za uongozi wao. Pia, historia inapobadilika ndivyo itikadi inavyobadilika katika jamii. Makala imeeleza dhana ya itikadi, imefafanua aina za itikadi na kuzibainisha katika tamthilia za *Maua kwenye Jua la Asubuhi* (2004) na *Kifo Kisimani* (2001). Baadhi ya aina za itikadi ambazo zimebainishwa katika tamthilia teule ni pamoja na; itikadi ya dini, ukombozi, utawala, itikadi ya utamaduni, itikadi ya umwinyi na itikadi ya ubepari. Aina hizi zimebainishwa kutokana na usemi wa wahusika na muktadha mazungumzo. Utafiti wa makala hii umeongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi (UTU) ilioasisiwa na Norman Fairclough (1989). Nadharia hii hueleza uhusiano uliopo kati ya matukio ya kisiasa, kiusemi, kiutamaduni, kimatini na kijamii. Huangazia athari ya itikadi katika matukio haya. Pia, huangazia jinsi usemi huo huathiri matukio haya katika jamii.

**APA CITATION**

Mugaduka, M. S. & Murithi, J. (2023). Itikadi Katika Tamthilia za Kifo Kisimani (2001) na Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2004) *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 84-100. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171.

**CHICAGO CITATION**

Mugaduka, Minyade Sheril and Jessee Murithi. 2023. “Itikadi Katika Tamthilia za Kifo Kisimani (2001) na Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2004)”. *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 84-100. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**HARVARD CITATION**
Mugaduka, M. S. & Murithi, J. (2023) "Itikadi Katika Tamthilia za Kifo Kisimani (2001) na Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2004)", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 84-100. doi: 10.37284/jammk.6.1.1171.

**IEEE CITATION**
M. S. Mugaduka & J. Murithi, "Itikadi Katika Tamthilia za Kifo Kisimani (2001) na Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2004)", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 84-100, Apr. 2023.

**MLA CITATION**
Mugaduka, Minyade Sheril & Jessee Murithi. "Itikadi Katika Tamthilia za Kifo Kisimani (2001) na Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2004)". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Apr. 2023, pp. 84-100, doi:10.37284/jammk.6.1.1171.

## UTANGULIZI

Itikadi ni dhana iliyo na maana nyingi. Eagleton (1991) ametaja baadhi ya maelezo ya dhana ya itikadi kama; mchakato wa kuunda maana, ishara na maadili katika jamii. Pili, itikadi ni mkusanyiko wa mawazo ya kundi fulani la kijamii au tabaka. Tatu; itikadi ni mawazo au fikra ambazo huhalalisha mamlaka ya kisiasa na seti za matendo zinazotekeleza vitendo. Eagleton (1991) anaendelea kueleza kuwa, itikadi hupata maana kutokana na mabadiliko ya kihistoria.

Marx na Engels (1977), wanaeleza itikadi kama fikra zote na maoni ya wanadamu kuhusu wanayosema na kufikiria kuhusu dini, sheria, siasa, uchumi na maadili. Itikadi ndiyo huelekeza namna mtunzi anavyosawiri maudhui na dhamira yake. Itikadi humwelekeza mwanadamu kuyatenda matendo mazuri au mabaya (Murithi, 2017). Mtindo na mbinu za uandishi huwa na athari za kiitikadi kama anavyotaja Fairclough (2001).

Makala hii imebainisha itikadi katika tamthilia teule za *Kifo Kisimani* na *Maua kwenye Jua la Asubuhi* zake Kithaka wa Mberia. . Dhana ya itikadi imeelezwa na aina za itikadi zimetajwa na kufafanuliwa kwa kina. Aina za itikadi katika tamthilia teule zimebainishwa kutokana na vipengele vya muktadha wa mazungumzo, usemi, na matumizi ya lugha. Vipengele hivi vimemwezesha watafiti kutambua maudhui ambayo yanaziweka wazi aina za itikadi. Aina za itikadi ambazo zimebainishwa katika tamthilia teule ni pamoja na; itikadi ya dini, ukombozi, utawala, itikadi ya utamaduni, itikadi ya umwinyi na itikadi ya ubepari

## NADHARIA

Makala hii imeongozwa na nadharia ya Uchanganizi Tahakiki Usemi (UTU). Nadharia ya UTU iliasisiwa na Fairclough Norman (1989) huko Lancaster School of Linguistics. Waitifaki wa nadharia hii ni pamoja na Wodak (1997) na Dijk (1998). Kwa mujibu wa Wodak (1997) UTU huangazia itikadi na utawala kutokana na data iliyoandikwa, inayoonekana, na iliyozungumzwa. Kulingana na Wodak, UTU huchukulia lugha kama tendo la kijamii na kuona muktadha wa lugha kuwa muhimu sana. Fairclough (2001) anaeleza kuwa UTU ni sayansi muhimu sana ya kijamii inayoangazia matatizo ambayo watu wanakumbana nayo kutokana na hali fulani ya maisha katika jamii na jinsi ya kuepuka matatizo hayo. Anaendelea kueleza kuwa dhana ya usemi huongozwa na itikadi. Mihimili ya UTU iliyoongoza utafiti wa makala hii ni; itikadi, utamaduni, usemi, viwango vya uchanganuzi na muundo wa jamii.

### Mbinu ya Utafiti

Utafiti wa makala hii ulifanyiwa maktabani. Watafiti walisoma tamthilia teule za *Maua kwenye Jua la Asubuhi* na *Kifo Kisimani*. Pia, walisoma vitabu na kupekea makala mtandaoni yanayohusiana na malengo ya makala hii. Dhana na aina za itikadi zimebainishwa kwa kujikita katika muundo wa kimaelezo. Tamthilia teule zilichaguliwa kimaksudi kutokana na uwepo wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

data ya kutosha. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo.

## MATOKEO NA MAJADILIANO YA UTAFITI

Katika sehemu hii, aina za itikadi zimefafanuliwa na kubainishwa kutoka katika tamthilia teule. Aina za itikadi ambazo zimebainishwa katika tamthilia teule ni pamoja na; itikadi ya dini, ukombozi, utawala, itikadi ya utamaduni, itikadi ya umwinyi na itikadi ya ubepari. Aina za itikadi zilizoainishwa ni kutokana na mawazo ya kijumla ya wataalam tofauti tofauti.

### Itikadi ya Dini

Dini ina maana nyingi kutegemea mitazamo ya wataalamu mbalimbali. Cosmstock (1984) anafafanua dini kama kile kilicho kitakatifu, uaminifu wa kuendeleza matendo mazuri, upendo kwa binadamu, na imani kwa miungu. Anaendelea kueleza kuwa dini ni kile ambacho tunakitenda bila kuonekana na kuilinda jamii. Aidha, Schilbrack (2013) anaeleza dini kama dhana inayotatua matatizo. Lakini ni matatizo yepi yanayofafanua matendo ya kidini yanapotatuliwa?

Dini ni sheria za kufanya na kutofanya ambazo mtu lazima azitumie ili ahesabiwe kuwa muumini mwaminifu. Dini ni imani inayohusiana na masuala ya kiroho. Suala la dini limezua mjadala kuhusu chanzo cha dini na imani. Plamenatz (1970) anaeleza kuwa katika dini, binadamu anajiona kama mtumwa wa kiumbe kilicho zaidi yake. Dini inamfanya kuamini kuwa yeye ni mtumwa na kuwa ni mwathiriwa wa mambo yaliyo zaidi yake. Ni mbinu potoshi ambayo lengo lake ni kukuza maadili kwa kutuza na kutishia adhabu ya maisha baada ya kifo. Kulingana na Plamenatz (ameshatajwa), dini ni fantasia ambayo huwafidia wanadamu kwa kushindwa kuwa na kile ambacho wanatamania kuwa nacho. Dini inaonyesha kiwango cha binadamu cha kutoelewa hali yake, iwapo angeelewa hali yake, basi hangeiambatanisha na dini.

Davis (1994) anaeleza dini kama mazoea ya kijamii. Kwa hivyo, dini inaathiri jamii kwa kuweka vigezo vya kukihukumu kile ambacho wanadamu wanakifanya katika jamii. Anaendelea kueleza kuwa, dini inasisitiza kuwa si kila jambo ambalo mwanadamu anafikiria na kutenda ni nzuri na lenye thamana. Imani ya dini katika jamii huzua utata inapotafsiri masuala ya ulimwengu nje ya ufahamu wa kiroho. Dini huonyesha kuwa utaratibu wa kijamii haukuanzishwa na binadamu bali kiumbe kilicho zaidi yake. Imani hii hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kama sehemu ya utamaduni. Davis (1994) anaonyesha matumizi ya lugha za kisiasa na matumizi mabaya ya lugha za kidini katika siasa. Wanasiasa wanatumia mfumo wa dini unaowaongoza wanadamu kuwadhulumu. Anatoa mfano wa Waisraeli ambao walitunukiwa ardhi takatifu na Mungu. Walitumia imani ya kupewa ardhi na Mungu kuhalalisha matendo yao na hali zao hasa kwa Wapalestina. Hata Waisraeli ambao hawakuwa wanathamini mambo ya Mungu, walitumia kigezo cha ‘kupewa ardhi na Mungu’ kwa sababu ya kujihalalisha.

Kwa mujibu wa Fitzgerald (2011), dini kwa jumla ni imani yenye sifa bia kuhusu uzoefu wa binadamu na taasisi. Anachukulia dini kama masuala ya kiroho na ‘ulimwengu mwingine’. Ni imani katika nguvu zisizo za kawaida. Dini ni upendo, amani, isiyopenda vurugu na isiyojihusisha na siasa. Fitzgerald anataja baadhi ya aina za dini kama dini ya Ukristo, Uhindu, Uislamu, na Ubudhi. Dini hizi zinaongozwa na itikadi tofauti tofauti. Kutokana na maelezo ya wataalam mbalimbali, dini ni mazoea ya kijamii yanayoyahusisha masuala ya kiroho na imani katika kiumbe kilicho zaidi ya binadamu. Matendo ya binadamu huongozwa na imani walionayo kwa kiumbe kilicho zaidi yao.

Katika tamthilia ya *Maua kwenye Jua la Asubuhi* (2004) suala la dini linadhihirika kutokana na muktadha wa mazungumzo kati ya Nyagachi, Kabitho, na Gachono (uk. 4-5). Itikadi ya dini imebainishwa kutokana na mhimili wa itikadi (Fairclough, 1989) ambao unashikilia kuwa usemi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

unafanya kazi ya itikadi. Kutokana na mazungumzo yao kuhusu changamoto walizokumbana nazo katika kambi ya wakimbizi. Visa vya kusambaza maradhi kuongezeka na ukosefu wa dawa. Usemi wa Kabitho kuhusu kulipiza kisasi unapelekea Gachono kupinga kauli hiyo kwa misingi ya imani ya dini yake kama inavyodhihirika katika nukuu uk 5:

> ***Kabitho:*** *Tutalipiza kisasi kwa namna ambayo hawataisahau milele.*
>
> ***Gachono:*** *Hakuna kisasi mtakacholipiza. Lakini Mungu atakisikia kilio chetu. Hatuna matumaini mengine. Mwenyezi Mungu pekee ndiye tegemeo letu.*

Kwa mujibu wa Fitzgerald (2011), ameeleza kuwa dini ni upendo, amani na isiyopenda vurugu. Gachono na Nyagachi hawataki vurugu kwa kulipiza kisasi, wanashikilia imani ya dini kuwa Mungu atakisikia kilio chao. Kutokana na muktadha wa mazungumzo haya, imani ya dini inadhihirika katika usemi wa Gachono. Kwa mfano, katika dini ya Ukristo, wanaamini kuwa kisasi hulipwa na Mungu kutokana na maandishi ya Biblia takatifu, katika kitabu cha Warumi 12:19.

> *'Wapenzi, msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu; maana imeandikwa, Kisasi ni juu yangu mimi; mimi nitalipa, anena Bwana.'*

Itikadi ya dini kuhusu kulipiza kisasi inajitokeza dhahiri katika vitabu vingine vya biblia mfano, kitabu cha Wahibrania 10:30 kinachoeleza kuwa kisasi ni chake Mungu na kuwa atakilipa na kuwahukumu watu wake. Katika kitabu takatifu cha dini ya uislamu suala la kisasi pia linaangaziwa. Quran 16:126 inaeleza kuwa;

> *'Ikiwa unalipiza kisasi, basi fanya hivyo kwa uwiano wa ubaya uliotendewa. Lakini ukivumilia basi ni bora kwa wanaovumilia.'*

Imani hii inawapa kina Gachono matumaini kuwa kuna kiumbe zaidi yao ambacho kinayatetea maslahi yao. Kwa kuzingatia mhimili wa itikadi (Fairclough, 1989), tunaonyeshwa imani ya Gachono inayojitokeza katika matendo yake na kuendelezwa kupitia kwa maombi. Nguvu za imani hii zinapelekea Gachono kumuomba mwenyezi Mungu awaondolee mateso wanayokumbana nayo ili wafurahie utukufu wake.

> ***Gachono:*** *Ewe Mungu, Muumba wetu, Mlinzi wetu. Geuza sikio lako, ewe mwenye enzi. Ulielekeze kwenye kilio chetu………Tazama nyuso zetu ambazo zimeloa machozi. Tuhurumie ewe mola……tuokoe kutoka kwenye mateso haya ili tuufurahie utukufu wako* (uk. 5).

Kama anavyoeleza Plamenatz (1970), dini inamfanya mwanadamu kuamini kuwa yeye ni mwathiriwa wa mambo yaliyo zaidi yake. Badala ya binadamu kujikomboa kutoka katika hali ile, ana imani kuwa Mungu mwenyewe atampigania na kumwondoa katika hali ile. Kutokana na mazungumzo kati ya Tungai, Gachono, na Nyagachi, imani yao inadhihirika kuhusu dini. Gachono na Nyagachi wanapomwelezea Tungai kuhusu masaibu yaliyowakumba, Tungai anawatia matumaini kuwa Mungu atasikia kilio chao.

> ***Tungai:*** *Msivunjike moyo. Lenye mwanzo lina mwisho. Mungu atasikia kilio cha Wandiku* (uk. 40).

Badala ya wao kujikomboa kutoka kwenye dhuluma za Watange, wanaamini Mungu atawapigania. Aidha, baada ya Tungai kukosa tikiti ya gari la kurudi Uganda, anaamini tukio hilo kuwa ni mpango wa Mungu ili awasaidie wakazi wa Lolomo Kaskazini. Anaamini kuwa kiumbe kilicho na uwezo zaidi yake ndicho chanzo cha hali aliyomo (uk 42). Usemi unaodhihirisha imani ya Tungai umebainishwa na mhimili wa muundo wa jamii (Fairclough, 1989). Kikwazo cha kijamii kilichotokana na kukosekana kwa mbinu ya kusafiri

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

kinapelekea Tungai kuzitumia semi zinazoiweka wazi imani yake.

> ***Tungai:*** *...pengine hayo ndiyo matakwa ya Mungu. Pengine hiyo ndiyo sababu nilikosa tikiti ya gari. Mungu anataka niwasaidie wakazi wa Lolomo kaskazini kujikinga kutokana na janga la maafa* (uk. 42).

Tukirejelea mawazo ya Plamenatz (1970), dini ni fantasia ambayo huwafidia wanadamu kwa kushindwa kuwa na kile ambacho wanakitamania. Ni imani ya kuwaliwaza tu ili waishi kwa matumaini. Mhimili wa usemi unaoonyesha ufungamano wa usemi na jamii unatumika kubainisha imani ya wahusika katika tamthilia ya *Kifo Kisimani* (2001). Imani ya dini imedhihirika katika usemi wa wahusika kama vile Mwelusi anapoeleza hali ya awali ya Butangi. Walikuwa na udongo wenye rotuba na walikuwa wanapata mazao ya kutosha. Anailinganisha na hali ya sasa ambapo njaa na Butangi zimekuwa kama chanda na pete. Ametumia usemi chanda na pete kusisitiza jinsi Wanabutangi wanavyoathiriwa na njaa. Gege anaamini kuwa hali hii haiwezi kubadilishwa na Mtemi Bokono kwa sababu njaa ni mpango wa Mungu (uk. 45-46).

Davis (1994) anataja kuwa maudhui chanya kuwa uongozi unatoka kwa Mungu yanatokana na uzoefu na maarifa ambayo hayana kikomo. Imani hii inahalalishwa na dini na hivyo kupekelea viongozi kuitumia ili kuhalalisha mbinu za uongozi wao. Anahitimisha kwa kueleza kuwa tatizo si matumizi ya lugha ya kidini katika siasa bali ni matumizi ya kisiasa katika lugha ya kidini. Kwa kutumikiza mhimili wa itikadi (Fairclough, 1989), itikadi ya dini imebainishwa kwa kuonyesha namna usemi unatumika kuonyesha muundo wa jamii wa kudumisha utawala usio sawa. Mtemi Bokono anatumia siasa katika lugha ya kidini. Kulingana na imani ya dini ya Kikristo, uongozi unatoka kwa mwenyezi Mungu na kila mtu anafaa kutii mamlaka. Wanaamini kuwa anayeasi mamlaka anashindana na agizo la Mungu na atajipatia hukumu (Warumi 13:1-2). Katika dini ya Uislamu, suala la kuheshimu mamlaka linasisitizwa katika Sura ya 4:59 katika Korani. Sura ya 4 inaeleza kuwa wanaoamini na kumuheshimu Mungu, Nabii, na wale walio katika uongozi na wanapokosana warejee katika sheria za Mungu. Katika mazungumzo kati ya Bokono, Batu, Zigu na Kame, tunaweza kutambua imani ya Bokono kuhusu anayepeana mamlaka. Katika usemi wake, anataja kuwa uongozi wake unatoka kwa Mungu aliyemketisha katika kiti cha enzi cha Butangi (uk.10). Mtemi Bokono anaendelea kueleza kuwa Mungu angependa aendelee kuiongoza Butangi kwa miaka mingi ili iendelee. Haya yanabainika kutokana na mhimili wa itikadi (Fairclough 1989) unaoonyesha imani ya jamii kuhusu utawala na watawala kama inavyobainika katika nukuu katika tamthilia ya *Kifo Kisimani* (2001) uk.10.

> ***Bokono:*** *Uongozi hutoka kwa Mungu. Mamlaka yangu yametoka juu. Mungu aliniketisha kwenye kiti cha enzi cha Butangi. Alifanya hivyo kwa mapenzi yake kwa Butangi. Nia yake ni kuona Butangi inaongozwa kwa Busara. Kwa hivyo aliniwekesha kwenye kiti cha Mtemi* (uk. 10)

Mtemi Bokono anatumia lugha inayoashiria imani ya dini katika kuendeleza siasa. Kutokana na usemi wake, anatumia imani ya dini kuhusu umbo la jamii linalohusisha masuala ya sheria na uongozi. Muundo wa jamii umeviweka bayana vikwazo vya kijamii vinavyopelekea kuweko kwa vyeo na hadhi. Walio uongozini wanafaa kuheshimiwa kwa sababu uongozi wao unatoka kwa Mungu.

Cavanaugh (2009) anauliza iwapo vurugu na vitisho ni sura ya dini au dini imeficha tabia za ndani za binadamu. Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*, kutokana na misingi ya imani kuwa uongozi hutoka kwa Mungu, Mtemi Bokono anaeleza kuwa Mungu angependa aongoze milele lakini kuna uchochezi. Anasisitiza kuwa uchochezi ni lazima ukomeshwe na Baraza la Wazee. Mawazo haya yanaoana na maoni ya Cavanaugh (2009) anayeuliza swali, “Je,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

vurugu ni sura ya dini?" Iwapo dini inaelekeza kuwa uongozi unatoka kwa Mungu, basi mbona Bokono anasisitizia Wazee wa Baraza kutumia vitendo ambavyo ni vurugu kukomesha uchochezi? *(uk 10).*

Plamenatz (1970), Davis (1994), na Cavanaugh (2009) wanachukulia itikadi ya dini kama imani inayotumiwa kuwapotosha wanadamu. Utaratibu wa kijamii ulioanzishwa na kiumbe kilicho zaidi ya binadamu unatumiwa kuficha tabia za ndani za binadamu na kumfanya kuamini kuwa yeye ni mwathiriwa wa mambo yaliyo zaidi ya uwezo wake. Mwelekeo wa mtunzi wa tamthilia za *Maua kwenye Jua la Asubuhi* na *Kifo Kisimani* unaoana na mawazo ya Plamenatz, Davis, na Cavanaugh kwa namna anavyosawiri imani ya wahusika kutokana na; muktadha wa mazungumzo na usemi unaoongozwa na itikadi. Mtunzi anaonyesha namna wahusika wanavyoendeleza vurugu na kuwakandamiza wenzao kwa misingi ya itikadi ya dini. Mwelekeo wa mtunzi ni kuwa dini inatumika kuendeleza uongozi mbaya na kuwapotosha wanajamii kutojikomboa kutoka kwa dhuluma.

**Itikadi ya Ukombozi**

Kulingana na maoni ya Montero (2009), ukombozi ni mchakato unaohusisha mabadiliko ya kijamii kwa lengo la kuleta usawa, kupinga ukandamizaji na dhuluma. Pia ukombozi huondoa taasisi zinazoendeleza maovu haya. Montero (keshatajwa), anaeleza kuwa ukombozi unaelekezwa katika sekta za kijamii zinazokandamizwa. Ukombozi unanuia kuwahamasisha watu kuhusu haki zao na umuhimu wa kuishi katika jamii yenye usawa na demokrasia.

Pavkovic (2005), anaeleza itikadi ya ukombozi kama seti ya imani, uamuzi wa thamani na maelekezo yanayoongoza hatua za kisiasa kwa lengo la kulikomboa kundi linalokandamizwa kutoka kwa watesi wao. Ili kudhibiti wanaodhulumiwa, watesi hutumia mbinu za kikatili. Anaendelea kueleza kuwa, wanaodhulumiwa hutumia nguvu na vurugu ili kujiondoa kutokana na ukatili wa watesi wao. Wakombozi wanaamini katika suala la kuleta haki katika malipo ya mshahara na kupewa nafasi sawa katika masuala yote ya kijamii pasi kudhulimiwa na viongozi wao.

Kwa mujibu wa Eddins (1972), ukombozi ni itikadi ya kisiasa ambayo inatoa mwongozo wa kuziunda sera za umma. Wakombozi wanaamini kuwa lengo kuu la sera za umma ni kuzilinda haki za wanaodhulumiwa na kuhakikisha usawa wa kukua na kujiendeleza kikamilifu. Aidha, Gramsci (1994) anaeleza kuwa ni vigumu kupata ukombozi. Wanaohitaji kukombolewa wamepewa majukumu na jamii kwa 'manufaa ya wote'. Wamezoea majukumu haya na kuyaona ya kawaida. Gramsci anaendelea kueleza kuwa wanajamii wanahitaji kufahamu na kuelewa nafasi yao katika historia, haki zao na wajibu wao. Anasisitiza umuhimu wa elimu katika kufikia ukombozi na haja ya elimu ya demokrasia. Kwake, elimu inawezesha jamii kidhibiti nguvu zinazowatawala na kupata ukombozi japokuwa itachukua muda mrefu kupata ukombozi.

Kutokana na maana tofauti tofauti za dhana ya itikadi ya ukombozi, ni dhahiri kuwa ukombozi unashughulikia haki za watu waliodhulumiwa na viongozi wao. Lengo la ukombozi ni kuwapa uhuru na uwezo wa kujiendeleza katika masuala yote ya kimaisha. Itikadi ya ukombozi inashikilia imani ya kujikomboa kutoka kwa uongozi mbaya. Kundi linaloshikilia imani hii linautekeleza mchakato huu kwa kuendeleza mapinduzi dhidi ya uongozi mbaya. Kitto (2019) anaeleza mapinduzi kama hatua muhimu ya kusaidia jamii kupata maendeleo kwa watu wa tabaka la chini kwa kuwaondoa mamlakani watu wa tabaka la juu na kuifanya jamii kuwa bila matabaka. Wanamapinduzi huondoa mfumo wa kibepari na kujenga ujamaa. Njogu (1997) anaeleza kuwa mapinduzi huweza kutokea kama watawala hawazingatii hali mbalimbali za kijamii, aidha kutokana na mapuuza au kutojali.

Mhimili wa viwango vya uchanganuzi (Fairclough, 1995) unaoangazia muktadha wa mahusiano ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

kijamii yanayoathiri usemi unatuelekeza katika kubaini itikadi ya ukombozi katika tamthilia ya *Kifo Kisimani (2001)*. Mahusiano kati ya Mwelusi, Bokono, na Wazee wa Baraza la Mtemi ni ya mvutano kuhusiana na uongozi mbaya. Mwelusi anaendeleza itikadi ya ukombozi, ana imani kuwa watakiuka kanuni ambazo ni za kikatili (*uk.83*). Baadhi ya kanuni ambazo anashabikia kupingwa ni pamoja na kanuni inayolitenga Bonde la Ilangi lisitumiwe na Wanabutangi. Atega anaeleza kuwa watapinga mpango wowote wa kugeuza Bonde la Ilangi kuwa mali ya Bokono na marafiki wake *(uk. 94).* Mawazo yake yanaungwa mkono na Mwelusi ambaye ana imani kuwa watakomboa kisima cha Mkomani na Bonde la Ilangi kwa manufaa ya Wanabutangi.

Usemi ni tendo la kijamii (Dijk, 1993). Usemi wa Mwelusi katika muktadha wa mazungumzo kati yake na Gege unaashiria imani yake ya kuikomboa Butangi. Katika uk.47, Mwelusi anaeleza kuwa anatumai kuwe na Butangi iliyo na usalama kwa wakazi wote, isiyo na njaa, inayozingatia haki na heshima kwa wote na kuwachukulia sawa watu wote. Kutokana na vikwazo vinavyoletwa na muundo wa kijamii, Mwelusi anataja tofauti zinazohusiana na ardhi, mila na utamaduni (uk.48) ambazo hazifai kuwa sababu za watawala kupendelea baadhi ya Wanabutangi. Anaongozwa na mawazo ya ukombozi wa Wanabutangi.

Katika tamthilia ya *Maua kwenye Jua la Asubuhi (2001),* itikadi ya ukombozi inatekelezwa kupitia kwa maandamano ya kupinga uongozi mbaya. Wahusika vijana wamesawiriwa kama wanaoyaendeleza mapinduzi. Usemi ni aina ya tendo la kijamii. Katika muktadha wa mazungumzo kati ya Nali na Tungai, Nali anatumia usemi maandamano kuashiria tendo la kijamii la kupinga chuki ya kikabila na uchochezi. Kupitia kwa maandamano, Tungai anawania kuwa watawafungua watu macho na kugundua kwamba viongozi wanawatumia tu kama inavyobainika katika nukuu hapa chini (*uk.79-80).*

> ***Nali:*** *... Nitashiriki katika maandamano kwa juhudi zote.*
>
> ***Tungai:*** *Maandamano gani?*
>
> ***Nali:*** *Maandamano ya kupinga chuki ya kikabila. Tumepanga kuandamana kupinga wendawazimu wa viongozi kuchochea wananchi dhidi ya wananchi wenzao.*
>
> ***Nali****: Sisi vijana. Mambo yakienda mrama nchini, sisi vijana vilevile watoto tutakuwa na dhiki kuliko watu wazima wanaochochea chuki….*

Kutokana na muktadha wa mazungumzo haya ni dhahiri kuwa Nali anaendeleza itikadi ya ukombozi. Ana lengo la kuwakomboa Watange na Wandiku dhidi ya vita vya kikabila.

Katika tamthilia ya *Maua kwenye Jua la Asubuhi (2004),* kabila la Wandiku likiongozwa na Tungai, Waito na Kabitho wanatafuta njia ya kukomesha vitisho dhidi ya kabila lao. Wanafanya hivi kwa kutaka kutafuta usaidizi kutoka kwa vikosi vya kulinda usalama na serikali. Wanaamini kuwa iwapo maandamano yatakomeshwa na rungu za polisi, basi njia nyingine ni kupeleka serikali katika mahakama ya kimataifa (*uk.70-71*). Waito anatumia neno maandamano kuonyesha itikadi waliyonayo dhidi ya uongozi kuwa pasi kutumia nguvu na vurugu basi serikali haitamakinika kama inavyodhihirika katika.

> ***Waito:*** *Kuna shida; hilo ni wazi kabisa. Lakini tukifuata njia mnayotaka kufuata, tutaleta shida kubwa zaidi. Tutumieni mbinu tofauti kukomesha vitisho dhidi ya kabila letu.*
>
> ***Kabitho:*** *Hatuhitaji mashauri yako.*
>
> ***Waito:*** *Nchi hii ina vikosi vya kulinda usalama. Ina mahakama. Ina serikali. Tuna haki ya kulindwa na serikali. Mbona tusitafute usaidizi wa serikali.*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

***Kabitho:*** *Kwa sababu wanaotaka kutuangamiza wanalindwa na serikali katika harakati zao.*

***Waito:*** *Tutafute namna ya kuishurutisha serikali kulinda haki zetu.*

***Tungai:*** *Na serikali utaishurutisha vipi?*

***Waito:*** *Zipo njia. Maandamano ya kila siku ni mojawapo ya njia* (uk. 70-71).

Mawazo ya Waito ya kutumia mandamano yanaoana na mawazo ya Pavkovic (2005) kuwa ili kujikomboa kutoka kwa dhuluma ya watesi, nguvu na vurugu hutumika. Anatueleza mawaidha yanayotoa uhalali kutokana na hatua za kisiasa kufanya maandamano au kupeleka serikali katika mahakama ya kimataifa.

Mwelekeo wa mtunzi wa tamthilia za *Kifo Kisimani (2001)* na *Maua kwenye Jua la Asubuhi* (2004) ni kuwa jamii inafaa kujikomboa kutokana na ukatili na ukandamizwaji. Kutokana na maudhui na matumizi ya usemi katika muktadha wa mazungumzo kati ya wahusika, mtunzi ameonyesha namna vijana wako katika mstari wa mbele katika kuendeleza mchakato wa kupata ukombozi. Mwelekeo wa mtunzi katika tamthilia teule unaoana na mawazo ya Montero (2009), Pavkovic (2005), na Eddins (1972) ambao wanashikilia kuwa itikadi ya ukombozi ni hatua ya kuleta usawa, kukomboa kundi linalokandamizwa na kudhulumiwa na kuunda sera zinazolinda haki za umma.

**Itikadi ya Utawala**

Utawala huendelezwa na suala la uongozi. Kwa mujibu wa Althusser (1981), sheria hutumiwa kuendeleza itikadi ya kiutawala wala si kuilinda haki. Aidha, mfumo wa kiutawala wa kidemokrasia ni mojawapo ya namna ya kuwanyamazisha watu wala si kwa maslahi yao. Uongozi waweza kuwa mbaya unaowanyanyasa wananchi kwa kuzuia haki zao za kidemokrasia. Wadhulumiwa huanza kutafuta mbinu za kujikomboa kutoka kwa utawala mbaya. Baadhi ya sheria ambazo huwekwa na watawala hutumiwa kuendeleza itikadi ya kiutawala.

Muya na Mwakagenda (2013) wamefafanua dhana ya utawala kama matumizi ya mamlaka ya kisiasa, kiuchumi au vinginevyo katika kusimamia masuala ya nchi kwa ngazi zote. Utawala waweza kuwa bora au mbaya. Wanafafanua utawala bora kama matumizi ya mamlaka yanayokuwa na uwazi, ushirikishaji wa watu, uwajibikaji, tija, ufanisi, uadilifu na usawa.

Mbatiah na Jagongo (2018) wanafafanua utawala kwa mikondo miwili; uongozi mzuri na uongozi mbaya. Uongozi mzuri unahusisha uwazi, uwajibikaji katika usimamizi wa mali ya umma. Wanaendelea kueleza kuwa wasomi wengi wanauchukulia utawala mzuri kama kigezo cha kuainisha athari zake katika kuboresha na kuimarisha uchumi.

Kwa mujibu wa Tangus na Sang (2020), utawala ni mfumo unaofafanua miundo inayotumiwa na mashirika au viongozi. Ni mfumo unaounda kanuni za kutetea haki na huwa na majukumu ya kuhakikisha mchakato wa usimamizi wa masuala yote ya kijamii ni mzuri. Wanaendelea kueleza kuwa, ni muhimu kwa mfumo wa utawala kushughulikia ngazi zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kutokana na fafanuzi tofauti tofauti za dhana ya utawala, ni wazi kuwa itikadi ya utawala inahusisha matumizi ya mamlaka katika kuboresha na kuimarisha nyanja zote za kijamii, kisiasa na kuichumi. Watawala wanatakiwa kuendeleza utawala mzuri unaopigania na kutetea haki za wanajamii na usawa katika ugawi wa rasilimali za jamii.

Katika tamthilia ya *Maua kwenye Jua la Asubuhi (2004)* tunapata kutambua imani ya Chebwe kuhusu utawala inayodhihirika kutokana na mazungumzo kati yake na Neche. Usemi unaotumiwa na Chebwe unaonyesha itikadi yake. Anatumia neno *kofia*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

kuashiria imani yake ya kutawala kama waziri. Kwa mfano:

> ***Chebwe:*** *Huvai kofia. Lakini hivi karibuni utakuwa ukiivaa. Utakuwa unaivaa kama wanawake wengine mashuhuri. Nimekununulia ili uzoee kuivaa mapema.*
>
> ***Neche:*** *Sielewi hata kidogo.*
>
> ***Chebwe:*** *Kuna dalili imara kabisa. Tutakuwa watu mashuhuri hivi karibuni. Dalili zanazoonyesha kwamba baada ya uchaguzi nitakuwa waziri. Nawe utakuwa mke wa waziri.*
>
> ***Chebwe:*** *Utakuwa unaivaa kwenye karamu na sherehe nyingine za waadhamu* (uk. 23).

Kanuni zinazowekwa na viongozi au watawala zinatumika kuwafunga watawaliwa kwa manufaa yao wenyewe. Mhusika Chebwe anauenzi sana utawala. Anatumia vijana kama vile Toiche katika mchakato wake wa kutaka kutawala. Anawafanya vijana hawa kula kiapo cha kupigana hadi wageni ambao wanataka kuchukua uongozi wa nchi waondoke. Haya yanatokana na mazungumzo kati ya Toiche na Chebwe:

> ***Toiche:*** *Nisipojiondoa, afya yangu itadidimia.*
>
> ***Chebwe:*** *Uliapa kwamba utapigana mpaka wageni waondoke Lolomo.*
>
> ***Toiche:*** *Niliapa. Lakini niliapa kutokana na habari ambazo hazikuwa sahihi. Mlitwambia kwamba Wandiku wanaunda vyama ya ili wachukue uongozi wa nchi kwa nguvu na kisha watupokonye mali zetu* (uk. 34).

Itikadi ni mojawapo ya mihimili ya uchanganuzi tahakiki usemi iliyotajwa na Fairclough (1989). Usemi hufanya kazi ya itikadi kwa kuonyesha imani ya jamii kutokana na utawala na watawala. Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani,* sheria zimewekwa na watawala ili kuwanyanyasa wananchi. Kutokana na muktadha wa mazungumzo kati ya Askari I, Askari II na Askari III, wanatumia usemi unaoashiria mawazo yao kuhusu kanuni za gereza:

> ***Askari I:*** *…Tumruhusu huyu mama amwone mwanae!*
>
> ***Askari III:*** *Tukifanya hivyo tutakuwa tunavunja kanuni za gereza.*
>
> ***Askari II:*** *Ambalo ni jambo baya sana!*
>
> ***Askari I:*** *Kanuni zinazomzuia mzazi kumwona mtoto wake ni kanuni ambazo zimepita mipaka.*
>
> ***Askari III:*** *Kanuni ni kanuni- ndani au nje ya mipaka!* (uk. 54).

Kutokana na muktadha wa mazungumzo haya, wahusika wanatofautiana kutokana na kanuni zilizowekwa na watawala. Askari I anaendeleza mawazo ambayo yanazipinga sheria ambazo zinamkandamiza mwananchi ilhali Askari II na III wanaunga mkono itikadi ya utawala inayokandamiza Wanabutangi. Aidha, utawala hufikia kikomo baada ya kipindi fulani cha wakati. Inaaminika kuwa hakuna mtu ambaye ataishi milele, na baada ya kiongozi kuaga, wengine huchukua hatamu za utawala. Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani (2001),* (uk.40), Askari I anaamini kuwa binadamu anapoaga, wanaopewa mamlaka ya kutawala wanaweza kuendeleza mfumo wa utawala wa hayati. Askari I anaimani kuwa utawala wa Mtemi Bokono utafikia mwisho na hali ya Butangi itabadilika.

Utawala unaendelezwa na siasa, kanuni na uongozi mbaya. Katika tamthilia ya Kifo Kisimani, Batu anaonyesha mawazo yake kuhusu utawala kutokana na usemi wake. Usemi anaoutumia unaonyesha namna baraza la Mtemi linatumia na linatekeleza utawala usio sawa. Batu anatumia semi kama siasa, uovu usio na kifani na mbinu za kunyamazisha wasioridhika. Maudhui ya uongozi mbaya yanajitokeza kati ya mazungumzo ya Bokono Batu na Zigu:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**Batu:** *Uovu usio na kifani? Siasa haina uovu usio na kifani. Kuna mbinu tu. Mbinu za kuwanyamazisha wasioridhika.*

**Zigu:** *Mbinu za kujikinga.*

**Bokono:** *Usipomnyoosha adui, adui atakunyoosha* (uk. 65).

Bokono ni mtawala wa Butangi akisaidiwa na Batu na Zigu. Mbinu ambazo wanatumia katika utawala wao zinawakandamiza Wanabutangi kama inavyodhihirika katika mazungumzo yao. Mazungumzo yao yameonyesha mahusiano ya kijamii na utawala yalivyojitokeza katika usemi wao (Dijk, 2001).

Kithaka wa Mberia ameonyesha mwelekeo wake kuhusu itikadi ya utawala kutokana na usemi na muktadha wa mazungumzo kati ya wahusika katika tamthilia za na *Kifo Kisimani (2001)* na *Maua kwenye Jua la Asubuhi (2004).* Mwelekeo wake ni kuwa watawala wanataka kuendelea kuongoza bila kujali maslahi ya wanajamii. Amejikita katika kuonyesha namna watawala wanatumia sheria katika kuendeleza itikadi ya kiutawala wala si kulinda haki (Althusser, 1981). Mfumo wa kiutawala unafaa kushughulikia ngazi zote za kisiasa, kijamii, na kiuchumi (Tangus & Sang, 2020) lakini watawala wanashughulikia ngazi hizi kwa manufaa yao binafsi.

## Itikadi ya Utamaduni

Utamaduni umefafanuliwa na wataalam mbalimbali kama vile; Mbaabu (1985), Adler (1997), Wamitila (2003), na Oatey (2008). Mbaabu (1985) anaeleza kuwa, utamaduni unahusu mila, asili, jadi na desturi za mavazi, vyakula, imani, tabia na maisha ya jamii kwa jumla. Adler (1997) anaeleza dhana ya utamaduni kama maarifa, imani, sanaa, maadili, sheria, desturi na mazoea ya kundi fulani la watu. Naye Wamitila (2003*)* anaeleza utamaduni kama uzoefu wa kimaisha wa watu fulani. Neno hili huleta pamoja michakato ya kijamii ambayo huiwezesha jamii kujieleza na kujitambulisha pamoja na kufanya shughuli za kila siku. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), utamaduni ni uzoefu wa kimaisha wa watu fulani. Usemi husheheni utamaduni wa jamii fulani. Aidha, kuna uhusiano kati ya usemi, jamii na utamaduni kama anavyotaja Dijk (2001).

Kulingana na Oatey (2008), utamaduni ni seti ya makisio na maadili, maelekezo ya maisha, imani, sera na kanuni zinazotumika na kundi fulani la watu. Kanuni na imani hii huathiri tabia na mienendo ya kundi hili na kulitofautisha na makundi mengine. Utamaduni ni muundo wa imani au mawazo yanayotofautisha kundi moja kutoka kwa makundi mengine.

Kuna uhusiano mkubwa kati ya usemi, utamaduni na jamii kwa mujibu wa Fairclough (1989). Usemi husheheni utamaduni wa jamii husika. Mwandishi wa tamthilia ya *Maua kwenye Jua la Asubuhi* (2004) ameonyesha suala la utamaduni kupitia kwa ukoo unaotokana na ndoa. Majadiliano ya mahari na harusi yanayotajwa ni masuala ya kitamaduni katika jamii ya Kiafrika. Kwa mujibu wa Nsereko (1975) kulipa mahari ni desturi kuwa mwanaume anafaa kupeleka mali kwa familia ya mke kabla ya kuoana. Hii ni ishara ya kushukuru waliomtunzia mke. Mahari huimarisha ndoa na kuhalalisha ukoo kati ya familia husika. Baadhi ya semi zilizotumiwa katika tamthilia teule kuashiria utamaduni huu ni; kuoa, mahari na harusi. Inaaminika kuwa kabla ya harusi, lazima kuwe na majadiliano ya mahari kama inavyojitokeza katika mazungumzo kati ya Kabitho na Tungai.

**Kabitho:** *Tungai umeoa nani?*

**Tungai:** *Wangane bila shaka.*

**Kabitho:** *Ndugu yangu, ndugu watumbo moja, ndugu wa toka nitoke. Wangane ni mtoto wa nduguye Kabitho. Kimila, mtoto wa dada au kaka au wa nduguye mtu, ni mtoto wa mtu huyo. Kwa hivyo Tungai* ***umeoa*** *binti yangu. Ulipokuwa ukijadiliana* **mahari** *ya Wangane….*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

> *siku ya harusi uliniona katika kundi la wakwe wako… mimi ni mkweo…* (uk. 16).

Muktadha wa mazungumzo kati ya Tungai, Nyagachi, na Gachoni katika boma la Tungai, suala la nyumba kuwa ya mke linadhihirika. Tungai anapowakaribisha nyumbani wanasita kuingia kwa sababu mwenye nyumba hayupo. Kama anavyoeleza Dijk (1993), usemi ni tendo la kijamii. Usemi wa Nyagachi na Tungai unaorejelea nyumba ni ya mke na ua wa nyumba ni wa mume mtawalia unaashiria uzoefu wa kijamii. Kama alivyotaja Wamitila (2003), utamaduni ni uzoefu wa kimaisha wa watu, ni uzoefu wa mwanamke kuwakaribisha wageni. Mhimili wa utamaduni (Fairclough, 1989) unabainisha itikadi ya utamaduni inayojitokeza katika usemi wa Nyagachi na Tungai kama inavyodhihirika:

> ***Tungai:*** *…karibuni. Ingieni nyumbani.*
>
> ***Nyagachi:*** *Mama watoto yumo?*
>
> ***Tungai:*** *Hayumo. Alienda sokoni.*
>
> ***Nyagachi:*** *Tutaingiaje nyumbani bila mwenye nyumba kuwepo?*
>
> *Nyumba ni ya mke*
>
> ***Tungai:*** *Natumai ua wa nyumba ni wa mume* (uk. 37)

Kama anavyotaja Wamitila (keshatajwa), utamaduni huwa uzoefu wa kimaisha wa watu fulani. Watu huwa na imani ambayo huwaelekeza kuendeleza uzoefu huo. Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani,* suala la utamaduni limedhihirika kutokana na semi zinazojumuisha ndoa, ngoma na nyimbo za kusifu viongozi. Suala la utamaduni wa ndoa linajitokeza kutokana na mazungumzo kati ya Gege, Mweke, na Talui (UK 69-70). Mweke anaelezea Gege jinsi alivyo na bahati kama ya mtende kwa sababu alifaa kuozwa bintiye Mtemi. Talui anakisia jinsi ***harusi*** ya Gege na Alida itakavyofana kuliko ile ya Dato na Mwelia. Mweke anaendelea kumwelezea Gege kuhusu ndoa yake na Alida katika uk. 73.

Utamaduni huendelezwa kupitia kwa nyimbo na ngoma. Mbaabu (1985) anataja utamaduni kama suala linalohusu mila, asili, jadi na desturi za mavazi, vyakula, imani, tabia na maisha ya jamii kwa jumla. Nyimbo na ngoma ni aina mojawapo ya utamaduni unaotambulisha desturi na tabia za jamii. Kulingana na Radocy na Boyle (1979), utamaduni huathiri aina ya nyimbo, vilevile, nyimbo huweza kuathiri utamaduni ambao unawasilishwa. Katika muktadha wa kisiasa, ni utamaduni wa viongozi kuimbiwa nyimbo za sifa. Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani (2001)*, usemi wa Tanya na Azena unaojitokeza kupitia kwa wimbo umesheheni utamaduni wa jamii. Tanya na Azena wanaeleza jinsi watu wanatiwa uoga ili waendelee kuimba nyimbo za kumsifu Mtemi Bokono kwa mfano:

> ***Tanya:***
>
> *Hekima ya mtemi bokono*
>
> *Kamwe haina mfano,*
>
> *Mapenzi yake kwa watoto*
>
> *Abadani hayana mwenza,*
>
> *Ujuzi wake wa uongozi*
>
> *Unametameta kama nyota,*
>
> *Na moyo wake wa ukarimu*
>
> *Ni kisima kisichokauka* (uk. 81).

Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani (2001),* ngoma imetumika. Ngoma ni sehemu ya utamaduni. Kaloo anataja kuwa viuno vitatingishwa mpaka viyeyuke na mojawapo ya ngoma ambazo zingechezwa ni chakacha (uk 3-4). Kutokana na muktadha wa mazungumzo kati ya Kaloo na Batu, wanatumia usemi ngoma. Usemi umesheheni utamaduni wa jamii na kufanya kazi ya itikadi. Matumizi ya ngoma katika muktadha wa mazungumzo yao

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

inaashiria hali ya uzoefu wa jamii yao wakati wa mikutano ya Mtemi:

> ***Batu:*** *...mambo yakoje upande wa ngoma?*
>
> ***Kaloo****: leo kuna maneno, viuno vitatingishwa mpaka viyeyuke.*
>
> ***Batu****: kama mafuta?*
>
> ***Kaloo****: kama mafuta karibu na moto.*
>
> ***Batu****: Barabara! Basi viuno na viyeyuke! Mtacheza ngoma gani?*
>
> ***Kaloo****: Kadha. Mojawapo ikiwa chakacha* (uk. 3-4).

Kutokana na mazungumzo haya, imani ya wahusika Batu na Kaloo kuhusu itikadi yao inadhihirika. Wanaamini katika utamaduni wa ngoma unaohusisha kutingishwa kwa viuno kwa lengo la kufurahisha Mtemi. Aidha, suala la utamaduni wa ngoma pia linadhihirika kupitia kwa Gege anayetumia semi zinazoashiria imani yake kuhusu ngoma. Katika uk 44, anaeleza kuhusu shughuli za kujenga jina lake katika ngoma.

Mwelekeo wa mtunzi katika tamthilia teule ni kuwa utamaduni unatumiwa kufikia malengo ya viongozi au watu binafsi kutokana na namna alivyosawiri wahusika na jinsi wanavyotumia usemi katika muktadha wa mazungumzo. Amejikita kwa namna uzoefu wa kimaisha wa watu fulani (Wamitila, 2003) unavyotumiwa na viongozi kuwadhalilisha wanajamii. Kwa mfano, utamaduni wa wimbo za kuusifu utawala mzuri kinyume na hali halisi.

**Itikadi ya Umwinyi.**

Kwa mujibu wa Holton (1985), dhana ya umwinyi ilitumika Ulaya kuanzia karne ya 16 kuendelea. Ilitumika kwa maana ya umiliki wa ng'ombe. Anaendelea kueleza kuwa itikadi ya umwinyi iliendelezwa na watu wenye nguvu ambao walimiliki mashamba. Wamiliki wa mashamba waliwadhulumu wakulima kwa kuwalipisha kodi na ushuru. Holton (1985), anasema umwinyi si mbinu ya uzalishaji bali ya kukuza ushikamano katika jamii. Anaendelea kueleza kuwa, mfumo wa umwinyi una mpango mzuri kwa wakulima na si unyanyasaji na umiliki wa mashamba kama inavyochukuliwa.

Wamitila (2003) anaeleza umwinyi kama mfumo wa kiuchumi ambao matajiri hurithishana utajiri wao huku wakimiliki mashamba makubwa pamoja na uwezo wa kisiasa. Kwa mujibu wa Hilton (1983), umwinyi unawakilisha muundo wa kijamii ambapo watawala wanatumia nguvu kupata mamlaka. Kwa hivyo, mbinu zinazotumiwa na mamwinyi kunyanyasa wakulima zinatokana na sababu za kisiasa bali si za kuujenga uchumi.

Martin (1986), anafafanua umwinyi kwa misingi ya kijamii na kiuchumi kuelezea uhusiano uliokuwepo kati ya mahafali waliofanya kazi kwa mashamba na wamiliki wa mashamba hayo. Ni mfumo ambao mahafali wanazalisha mali lakini mazao yao yanachukuliwa na mamwinyi. Martin anaeleza kuwa, katika mfumo huu, mahafali wanaozalisha mali wanatenganishwa na mazao hayo. Wamiliki ndio wanaodhibiti kiwango cha ardhi kinachotumiwa na mahafali na mbinu zote za malipo kwa kuwatoza ada za juu.

Kutokana na maelezo ya wataalam mbalimbali, itikadi ya Umwinyi ni mfumo ambao matajiri wanamiliki na kudhibiti mashamba makubwa. Mahafali hutumiwa na matajiri hawa kuzalisha mali lakini wanatenganishwa na mazao yao kwa kupimiwa kiwango cha ardhi wanachoweza kukitumia na kuwatoza ushuru na ada za juu.

Katika tamthilia ya *Mau kwenye Jua la Asubuhi* (2004), Kabitho anadai kuwa anatetea haki za Wandiku wenzake ilhali anaendeleza mfumo wa kimwinyi. Iweje Wandiku wenzake hawana makao ilhali ana mashamba makubwa. Wanalalia udongo baridi na watoto wao wanakufa ilhali Kabitho hana habari kuhusu vifo hivyo. Muundo wa kijamii umeleta vikwazo vya kitabaka ambapo tabaka la juu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

la Kabitho linamiliki mashamba ekari zaidi ya mia hamsini ilhali tabaka la chini linalowakilishwa na kina Nyagachi hawana makao, ni maskuota. Kama inavyodhihirika katika mazungumzo kati ya Kabitho na Tungai:

> ***Kabitho:*** *Hawajambo. Wote wako katika shamba la Buratu. Wamekwenda kusimamia uvunaji wa viazi na pareto. Mimi pekee ndiye nimebaki hapa.*
>
> ***Tungai:*** *Huku umepanda nini?*
>
> ***Kabitho:*** *Ngano katika ekari mia na hamsini. Katika sehemu iliyosalia nimepanda sayari* (uk. 7).

Ili kushadidia mfumo wa umwinyi unaoendelezwa na Kabitho. Kutokana na mazungumzo kati ya Nyagachi, Kabitho na Gachono, tunatambua madhara ya mfumo huu. Nyagachi anaeleza jinsi walivyofukuzwa katika mashamba yao. Anamwuliza Kabitho iwapo kuwatembelea kutawarejeshea mashamba yao. Kwa kutetea imani yake, Kabitho anawaeleza kuwa wanafanya mipango ya kuwarejeshea mashamba yao.

Mazungumzo kati ya Nali, Nche, na Chebwe yanadhihirisha namna umwinyi umekita mizizi. Walio na ardhi kubwa hawaitumii kujenga uchumi ilhali wenzao hawana hata futi kumi. Muundo wa kijamii umepelekea kuundwa kwa semi maskuota unaoonyesha mgawanyiko wa matabaka. Nali anatumia neno *maskuot**a*** kuashiria wale ambao wanakaa katika ardhi ambayo si yao bila idhini ya mwenye ardhi hiyo kama inavyodhihirika:

> ***Nali****: Baba, kuna Wandiku wengi ambao hawana hata ekari moja…*
>
> ***Nali; ….*** *Watu wachache wana ekari maelfu wakati wengine hawana hata futi kumi mraba za udongo. Baadhi ya wenye ardhi hiyo kubwakubwa hawaitumii ili kuchangia uchumi wa nchi…Tuna Maskuota wengi* (uk 60-61).

Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani (2001)*, mtunzi ameonyesha itikadi ya umwinyi kupitia kwa Mtemi Bokono. Aidha, ameonyesha pia wanaopinga mfumo huu kupitia kwa mhusika Nyalwe. Kama ilivyotajwa awali, muundo wa kijamii huchunguza vikwazo vya kijamii kama vile tabaka, cheo na hadhi. Kutokana na mhimili huu, tunatambua namna cheo na hadhi vinatumika kuendeleza mfumo wa umwinyi. Wahusika wamepewa vyeo kama Askari Mkuu na Mgawa Ardhi kama anavyotaja Nyalwe. Mgawa ardhi anauendeleza mfumo wa umwinyi kwa kumrithisha Askari mkuu ardhi ya wanakijiji wanaowakilishwa na Mama Agoro kama inavyodhihirika:

> ***Nyalwe:*** *Ninayoyazungumza ni muhimu. Usinitie mzaha! Mama Agoro alikuja kulalamika. Anasema uwanja wa kuchezea watoto wao umechukuliwa. Umepewa Askari Mkuu.*
>
> ***Bokono:*** *aliyempa Askari Mkuu ni nani?*
>
> ***Nyalwe:*** *Mgawa Ardhi.*
>
> ***Bokono:*** *Basi kwa nini alikuja hapa badala ya kwenda kwa mgawa ardhi?*
>
> ***Nyalwe:*** *Wafanyakazi wanapopuuza kanuni zinazoongoza mamlaka yao, sharti mkubwa wao akumbushwe kuzingatia kanunu hizo.*
>
> ***Bokono:*** *Mgawa ardhi amepuuza kanuni gani?*
>
> ***Nyalwe:*** *Kanuni zinazolinda ardhi ya umma* (uk. 18-19)

Muktadha wa mazungumzo kati ya Bokono na Nyalwe unaashiria itikadi ya umwinyi inayoendelezwa na wahusika waliopewa majukumu ya kutetea kanuni za kuilinda ardhi ya umma. Kama anavyoeleza Holton (keshatajwa), mfumo wa umwinyi unaendelezwa na watu wenye nguvu wanaowadhulumu watu wa tabaka la chini.

Kwa namna anavyowasawiri wahusika, mtunzi wa tamthilia teule ameonyesha mwelekeo wake

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

kuwahusu wahusika walio na uwezo na mamlaka wanavyomiliki mashamba makubwa na uwezo wa kisiasa. Imani yake kuhusu mfumo wa umwinyi inaonyesha muundo wa kijamii unaowapa watawala mamlaka na nguvu za kurithi na kudhibiti mashamba huku wanajamii wakiachwa bila ardhi.

**Itikadi ya Ubepari**

Mfumo wa ubepari uliibuka kutokana na mfumo wa umwinyi kulingana na mawazo ya Marx (1941). Aidha, Anderson (1979) anapinga kauli kuwa umwinyi ndicho chanzo cha ubepari. Anderson anachukulia ubepari kama mfumo unaohusisha maendeleo ya kiuchumi kutokana na sifa za kupanuka kwa mbinu fulani ya uzalishaji. Kulingana na Holton (1985), kuibuka kwa mbinu za uzalishaji za kibepari na kukua kwake katika enzi za viwanda, kulitegemea mbinu zilizokuwepo awali. Anaendelea kueleza kuwa ubepari si ishara ya uhuru wa kiuchumi bali ni ishara ya unyonyaji na mzozo wa kimadaraka katika nyanja ya uzalishaji. Ubepari ni mfumo wa kiuchumi, kisiasa na kijamii wa umiliki binafsi wa mali, biashara na viwanda kwa lengo la kutengeneza faida kubwa na baadhi ya watu binafsi kufaidika. Mabepari hutumia mahafali kujifaidi.

Laclau (1979), anataja kuwa ubepari unahusisha mambo yafuatayo; mfumo wa uzalishaji kwa soko, faida ndicho kichocheo cha uzalishaji na mwisho, faida hii hupatikana kwa manufaa ya mtu mwingine ila si mzalishaji.

Amin (2011) anaeleza ubepari kama kutokuwepo kwa usawa unaotokana na mahusiano ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Anataja mfumo wa ubepari kama kinyume cha uhusiano wa utawala kati ya vyombo vya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Kutokuwepo kwa usawa huu kunapelekea kuibuka kwa soko mpya zinazotawaliwa na mabepari wanaotawala uzalishaji wa kijamii na kutoza kodi za juu. Amin (2011) anaendelea kueleza kuwa mabepari ambao ni asilimia 20% wanahitaji mahafali ambao ni 80% kujinufaisha kutokana na mikondo yote ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Aidha, mfumo huu hauunganishi tu watu wa taifa moja bali ni mfumo unaounganisha ulimwengu. Kutokana na maelezo haya, itikadi ya ubepari inahusisha mfumo wa uzalishaji wa kiuchumi, kijamii, na kisiasa unaomilikiwa na watu wachache kwa manufaa yao binafsi. Mabepari wanaongozwa na imani ya kutumia mahafali katika mchakato wa uzalishaji lakini hawahusishwi na faida ya mazao ya uzalishaji wao. Mahafali hawana uwezo wa kujiendeleza kiuchumi kutokana na sheria kali zilizowekwa na mabepari katika mikondo yote ya kiuchumi na kisiasa.Ubepari unahusisha mfumo wa kiuchumi. Murithi (2017) anaeleza uchumi kama jumla ya shughuli zote za binadamu zinazolenga kutosheleza mahitaji ya watu. Mfumo wa kiuchumi unahusisha uzalishaji, usambazaji, utumiaji wa bidhaa na kutolewa kwa huduma mbalimbali.

Katika tamthilia ya *Maua kwenye Jua la Asubuhi (2004)*, kutokana na mazungumzo kati ya Gachono, Nyagachi, na Kabitho, tunatambua namna uchumi ulivyozorota. Kwa kuzingatia viwango vya uchanganuzi vinavyoangazia muktadha wa mahusiano ya kijamii ambayo huathiri usemi, semi zinazoashiria hali duni ya tabaka la chini zinatumiwa. Kuwepo kwa viroboto, upungufu wa chakula na vifo vya akina mama na watoto ni matokeo ya watu fulani kujilimbikizia mali ya umma. Katika uk 2, Nyagachi anaeleza kuwa walifukuzwa katika mashamba yao. Hawana hati ya ardhi yao kwa sababu zilitafunwa na mioto. Ni desturi kuwa na hati ya umiliki wa ardhi kama Ushahidi kuwa ardhi ile ni ya mtu fulani. Wanaamini kuwa iwapo hawana hati hizo basi itakuwa vigumu kupata ardhi waliyonyang'anywa kama inavyothihirika:

> ***Gachono:*** *Vitazame vibanda tunamolala. Tazama plastiki nyeusi zenye* ***matundu makubwa kama vinywa vya pango***
>
> ***Nyagachi:*** *Tunalalia udongo baridi. Viroboto watunyonyao damu wamenona na kuwa Wakubwa kama panya.*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

> ***Gachono:*** *…. Baridi kali. Baridi inayochoma kama moto.*
>
> ***Nyagachi:*** *Watoto wanakufa kutokana na nimonia. Na bado kaburi hazijafunga milango* (uk. 2-3).

Gachono anatumia tashbihi kusisitiza hali ya Wandiku waliofukuzwa kutoka kwa ardhi yao. Kwa mfano; baridi inayochoma kama moto. Wanailinganisha hali hiyo kuonyesha uzito wake kama inavyodhihirika katika maneno yaliyokolezwa katika mazungumzo ya hapo juu. Aidha, hali hii inaoana na mawazo ya Amin (2011) kuwa mfumo wa ubepari unazuia ustaarabu wa binadamu.

Mfumo wa kiuchumi na kijamii unafaa kuwanufaisha wanajamii wote. Aidha, katika tamthilia ya *Kifo Kisimani* ni kinyume na haya. Mabepari wanajinufaisha kutokana na mikondo yote ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, (Amin, 2011). Usemi ni tendo la kijamii (Dijk, 1993), kutokana na usemi wa Andua, tunatambua namna itikadi ya ubepari inavyoendelezwa. Wanakijiji hawaruhusiwi kuchota maji kwenye kisima cha Mkuyuni. Kutokana na mazungumzo kati ya Andua na Tanya (UK 49), inadhihirika kuwa, maji ya bwawa ambayo yanafaa kutumika kwa manufaa ya wanadamu, yameachiwa ng'ombe wa mwanawe Mtemi. Badala ya ngombe wale kuchotewa maji, wanaachiliwa ndani ili wanywe moja kwa moja kutoka bwawani. Andua anaeleza jinsi askari waliwapiga kwa sababu ya kuchota maji kisimani mmoja wao akamsukuma na kuangukia jiwe akaumia.

Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani (2001)* usemi wa Gege unaashiria tendo la kijamii la kujilimbikizia mali bila kuwajali wengine. Usemi wake unaingiliana na mawazo ya Anderson (1979) anayeeleza kuwa ubepari unahusisha maendeleo binafsi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Katika uk 47, Mwelusi anapoeleza kuwa binadamu anafaa kuyaboresha mazingira ili aweze kutatua matatizo ya jamii, Gege anamwelezea kuwa badala ya kufikiria njia za kujichumia mali na kujifurahisha maishani, anajihangaisha kwa kufikiria jamii. Kutokana na matamshi ya Gege, inadhihirika kuwa anaamini kwa kujitajirisha na kujikuza kiuchumi bila ya kuwajali wengine.

Mwelekeo wa mtunzi wa tamthilia za *Kifo Kisimani* na *Maua kwenye Jua la Asubuhi* (2004) kuhusu itikadi ya ubepari unaashiria maendeleo binafsi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa, (Holton, 1985). Mtunzi amedhihirisha mwelekeo hasi kuhusu mfumo wa ubepari kutokana na namna alivyo tumia usemi kusisitiza ubinafsi wa baadhi ya wahusika katika kujiendeleza. Mabepari hawajali maslahi ya watu wengine bali yao tu. Wanachochewa na faida zinazotokana na uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma. Mtunzi ameonyesha namna wanajamii wanavyoathirika na mfumo huu unaozuia ustaarabu wa binadamu, (Amin, 2011).

## HITIMISHO

Katika makala hii, dhana ya itikadi imefafanuliwa kama fikra zote na maoni ya wanadamu kuhusu wanayosema na kuyafikiria kuhusu masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Aina za itikadi zimebainishwa katika tamthilia za *Kifo Kisimani* (2001) na *Maua kwenye Jua la Asubuhi (2004*). Baadhi ya aina za itikadi zilizobainishwa ni itikadi ya dini, utawala, utamaduni, umwinyi, ubepari na ukombozi. Watafiti wameonyesha aina za itikadi kwa kujikita katika muktadha wa mazungumzo, usemi, maudhui na uhusiano uliopo kati ya wahusika. Imani katika jamii kuhusu hali ya maisha inadhihirika katika usemi wa wahusika. Usemi ni aina ya tendo la kijamii.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

**MAREJELEO**


Adler, N. (1997). *International Dimensions of Organizational Behavior*. (3rd ed). Ohio. South-Western College Publishing.

Althusser, L. (1981). Ideology and Ideological State Apparatuses. In *Lenin and other Essays* (B. Brewster, mtaf). London. New Left Books.

Amin, S. (2011). *Ending the crisis of capitalism or ending capitalism?* Nairobi. Pambazuka Press.

Anderson, P. (1979). *Passages from Antiquity to Feudalism*. London. New Left Books.

Cavanaugh, W. T. (2009). *The Myth of Religious Violence*. New York. Oxford University Press.

Cosmstock, W. R. (1984). Toward Open Definitions of Religion. *Journal of the American Academy of Religion*, *52*(3), 499–517. http://www.jstor.org/stable/1464205 . Imepakuliwa tarehe 10 Juni 2022.

Davis, C. (1994). *Religion and the Making of Society*. New York: The Press Syndicate of Cambridge University.

Dijk, V. (1998). *Ideology. A multidisciplinary Approach.* London: Sage Publication.

Dijk, V. (1993). *Principles of Critical Discourse Analysis in: Discourse and Society*. London: Sage Publication.

Dijk, V. (2001). *Multidisciplinary CDA*: A Plea for Diversity in Ruth Wodak and Michael Meyer (eds) *Methods of Critical Discourse Analysis*, uk. 95–120. London: Sage.

Dijk, V. (2003). A Framework for Digital Divide Research. *Electronic Journal of Communication*, 12(1,2). https://research.utwente.nl/en/publications/a-framework-for-digital-divide-research.

Eagleton, T. (1991). *Ideology: An introduction.* London: Verso.

Eddins, B. B. (1972). Liberalism and Liberation. *Social Theory and Practice*, *2*(1), uk 99–112. http://www.jstor.org/stable/23556671.

Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. London. Longman Publishers.

Fairclough, N. (1995). *Critical Discourse Analysis: Study of Language*. London: Longman Publishers.

Fairclough, N. (2001). *Language and Power* (2nd ed.). New York. Routledge. https://doi.org/10.4324/9781315838250. Imepakuliwa tarehe 12 Machi 2022.

Fitzgerald, T. (2011). *Religion and Politics in International Relations: The Modern Myth*. London: Bloomsbury.

Gramsci, A, Bellamy. R. (ed). (1994). *Pre-Prison Writings.* London. Cambridge University Press.

Hilton, R. (1983). *Feudal society*. In T. Bottomore et, al. (Ed.). *Dictionary of Marxist Thought*. Oxford. Blackwell company.

Holton, R. J. (1985). *The Transition from Feudalism to Capitalism.* London. Macmillan Publishers

Kithaka wa Mberia. (2001). *Kifo Kisimani*. Nairobi. Marimba Publications.

Kithaka wa Mberia. (2004). *Maua kwenye Jua la Asubuhi*. Nairobi: Marimba Publications.

Kitto, I. B. (2019). *Kuchunguza Siasa na Itikadi katika Tamthilia ya Nyota ya Mboya*. [Tasnifu haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania].

Laclau, E. (1979). Politics and ideology in Marxist theory: Capitalism and Fascism. London: Lowe & Brydon Printers.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1171

Larrain, J. (1979). *The Concept of Ideology*. London: Hutchinson &Co. Publications Ltd.

Marx, K. (1941). *Pre-Capitalist Economic Formations.* New York: International publishers.

Marx, K. & Engels, F. (1977). *The German Ideology*. London: Lawrence and Wishart.

Martin. E. J. (1986). Feudalism to Capitalisim. Peasant and Landlord in English Agrarian Development. London. Macmillan Press.

Mbatiah. J. & Jagongo. A. (2018). Good Governance, Development Expenditure and Economic Growth: Theoretical Review. *International Journal of Management and Commerce Innovations* Vol. 5, Issue 2, uk: (802-809), October 2017 - March 2018. Ilipakuliwa tarehe 21 Juni 2022.

Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili*: Kenya. Publishing and Book Marketing C.O ltd.

Montero, M. (2009). Methods for Liberation: Critical Consciousness in Action. In: Sonn, C., Montero, M. (eds) *Psychology of Liberation.* Peace Psychology Book Series. Springer, New York, NY. https://doi.org/10.1007/978-0-387-85784-8_4. Ilipakuliwa tarehe 25 Agosti, 2022.

Murithi, J. (2017). Itikadi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed. [Tasnifu Chuo Kikuu cha Kenyatta. haijachapishwa].

Muya, I. F. & Mwakagenda. H. (2013). Mwongozo wa Utawala Bora. Policy Forum. Toleo la Kwanza September 2013. Dar es Salaam. Tanzania Printers Limited. https://www.policyforum-tz.org/sites/default/files/UtawalaBora_0.pdf. Ilipakuliwa tarehe 25 Agosti 2022.

Njogu, K. (1997). *Uhakiki Wa Riwaya Za Visiwani.* Nairobi. University of Nairobi Press.

Nsereko, D. D. (1975). The Nature and Function of Marriage Gifts in Customary African Marriages. *The American Journal of Comparative Law*, *23*(4), 682–704. https://doi.org/10.2307/839241. Ilipakuliwa tarehe 2 Novemba 2022.

Pavković, A. (2005). Terrorism as an instrument of liberation: a liberation ideology perspective. Katika G. Meggle (Ed.), *Ethics of terrorism and counter-terrorism* (uk. 245-260). OntosVerlag. https://doi.org/10.1515/9783110 327496.253. Ilipakuliwa tarehe 2 November 2022.

Plamenatz, J. P. (1970). *Ideology*. London: Macmillan publishers.

Radocy, R., & Boyle, J. D. (1979). *Psychological foundations of musical behavior.* Illinois, United States of America, C. C. Thomas.

Schilbrack, K. (2013). What Isn't Religion? *The Journal of Religion*, *93*(3), 291–318. https://doi.org/10.1086/670276. Ilipakuliwa tarehe 12 Mei 2022.

Oatey, S. H. (2008) Culturally Speaking. Culture, Communication and Politeness Theory. 2nd edition. London: Continuum.

Tangus. C & Sang. P. (2020). Linking Governance to Performance of Government-funded Projects in Kenya. *The International Journal of Business & Management*. Vol 8 Issue 11 uk 45. November, 2020.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi Ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wodak, R. (1997). *Gender and Discourse*. London: Sage Publications.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.